

Kuweka Picha Mtandaoni Kunaathirije Sifa Yako?

Jipime kupitia mifano ifuatayo.

MFANO WA 1

Wewe ni msimamizi wa kampuni kubwa ya biashara, na ungependa kuajiri vijana. Kwa kuwa watakuwakilisha wewe na kampuni yako, unatarajia vijana utakaowaajiri wawe na tabia nzuri.

Sasa, mfikirie mmoja kati ya rafiki zako. Wazia yeye ndiye amekuja kwako kuomba kazi. Andika jina la rafiki yako unayefikiria kumwajiri.



Jina: _____



Je, atasaidia au ataharibu sifa ya kampuni yangu?

Kwa kutegemea mambo ninayoona, je, ninaweza kumwajiri?



MFANO WA 2

Unakwenda kufanya mahojiano ya kazi. Mwanamume unayetarajia atakuwa mwajiri wako ni msimamizi wa kampuni kubwa ya biashara. Angependa kuwaajiri vijana. Kwa kuwa wote anaoajiri watamwakilisha yeye na kampuni yake, anatarajia wawe na tabia nzuri.

Ikiwa utamruhusu achunguze akaunti yako ya mtandao wa kijamii—ukiwa na matarajio ya kuajiriwa naye—andika mambo unayofikiri mwajiri huyo anaweza kufikiria kwa kutegemea picha ulizotuma au kutumiwa na maelezo uliyotoa kwenye mtandao huo wa kijamii.



Picha zinaweza kutoa mawazo tofauti kuhusu mtu. Kwa mfano, mtu kwenye picha iliyo juu anaweza kuonwa kwa njia mbili.

A. Jasiri

B. Asiyejali

Katika picha zilizo hapa chini, andika mambo mawili yanayoweza kufafanuliwa kuhusu sifa ya mtu huyo.



A. _____

B. _____



A. _____

B. _____

